

Taasisi yadai uchumi safi


■ Fredy Azzah

TAASISI ya Utafiti wa Kiuchumi na Kijamii (ESRF), imesema kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita, serikali imejitahidi kutekeleza malengo ya dira ya taifa ya 2025, na kuwa changamoto ilivopo sasa ni kuweka ubora katika mipango iliyotekelzwa.

Hayo yalibainishwa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mkuu wa ESRF, Dk Hoseana Lunogelo, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari juu ya shughuli ya kupima na kukusanya mawazo ya wadau kuhusu hatua iliyofikiwa katika kutimiza Dira ya Taifa ya 2025, jukumu ambalo taasisi hiyo imepewa na serikali.

Dk Lunogelo alisema katika baadhi ya sekta ya maeneo ikiwa ni pamoja na elimu, utawala bora, pamoja na uchumi, serikali imepiga hatua kidogo.

Baadhi ya malengo ya Dira ya Taifa ya 2025, ambayo kwa sasa imebaki miaka 15 kufikia mwisho wake, ni kuhakikisha maisha ya Mtanzania yanaboreka na kupata kipato cha angalau dola 3000 za Marekani kwa mwaka ambazo ni sawa na Sh 10,000 kwa siku. Pamoja na mafanikio hayo, Dk Lunogelo alisema ubora katika shughuli zote zilizofanyika, unatakiwa kuwa moja ya shughuli zitakazofanyika kwa kipindi cha miaka 15 iliyobaki.



Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kiuchumi na Kijamii (ESRF), Dk Hoseana Lunogelo akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam kuhusu tathimini ya Mpango wa Taifa wa Dira ya Maendeleo 2025. Picha na Fidele Felix.